

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Anwani: "AFYA", DODOMA
Simu Na: + 255 – 026 - 2323267
Nukushi:
(Barua zote ziandikwe kwa: KATIBU MKUU)



Chuo Kikuu cha Dodoma.
Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya Maendeleo ya Jamii
Jengo Na. 11
S.L.P. 743
40478 DODOMA

Unapojibu Tafadhali taja:

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU UTAFITI WA KITAIFA WA
HALI YA LISHE NCHINI ULIOANZA KUFANYIKA TAREHE 24 SEPTEMBER 2018
NA UTAKAO ENDELEA HADI NOVEMBER, 2018**

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto kupitia Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya – Zanzibar, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Zanzibar (OCGS) inaendesha Utafiti wa Kitaifa kwa lengo la kubaini hali ya Lishe nchini. Utafiti huu umeanza mwezi Septemba na unatarajiwa kukamilika Novemba 2018, ukitumia methodolojia iitwayo SMART ikiwa na maana ya ukusanyaji wa takwimu na uchambuzi wake kwa wakati na kuchukua hatua stahiki ili kutatua matatizo yaliyopo kwa sasa na kuandaa mazingira ya kujikinga na matatizo hayo. Utafiti huu hufanyika kipindi cha kati baada ya kufanyika kwa utafiti mkubwa wa kitaifa wa Afya na Demografia ambao hufanyika kila baada ya miaka mitano.

Utafiti wa kwanza wa aina hii ulifanyika mwaka 2014 kufuatia utafiti wa Afya na Kidemografia uliokuwa umefanyika mwaka 2010. Utafiti huu ni wa pili na utafanyika katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara pamoja na Mikoa 5 ya Zanzibar. Katika kila Mkoa, sampuli ya kaya zitachaguliwa kushiriki kwa kufuata utaratibu maalum wa kitaalamu, ili kuziwakilisha kaya nyingine katika eneo linalochaguliwa katika kila Wilaya. Utafiti huu utahusisha zaidi ya kaya 18,000 ambapo jumla ya watoto 14,000 walio kwenye umri wa chini ya miaka mitano na wanawake walio kwenye umri wa kuzaa wapatao zaidi ya 10,000 watahusika katika utafiti huu. Pia jumla ya sampuli 10,000 za chumvi inayotumika katika kaya zitazofikiwa zitapimwa ili kubaini kiwango cha madinjoto kilichomo kwenye chumvi.

Utafiti huu unalenga kutathmini hali ya lishe katika jamii zetu, hususani; kubaini hali ya lishe miongoni mwa watoto wenye umri kuanzia umri wa miezi 0 hadi 59; miongoni

mwa wanawake walio katika umri wa kuzaa, yaani miaka 15 hadi 49; Kubaini hali ya utoaji wa matone ya vitamini A na madini chuma / asidi ya foliki, dawa za kuzuia minyoo; matumizi ya chumvi iliyo na madinjoto; kutathmini hali ya viwango vya upungufu wa damu miongoni mwa wanawake walio katika umri wa kuzaa; pamoja na hali ya usafi mazingira katika kaya (hususani tabia na desturi za kunawa mikono).

Ushiriki katika utafiti huu ni wa hiyari, na baada ya wahusika katika kaya kuridhia ndipo watafiti wetu wataendelea na zoezi la utafiti. Taarifa zote zitakazotolewa pamoja na majibu watakatoyatoa wahusika katika maswali watakatoyulizwa yatahifadhiwa kwa usiri mkubwa. Washiriki wote katika utafiti huu watanufaika kwa kutambua hali zao za lishe. Kwa upande wa watoto walio na umri chini ya miaka 5 wenye utapiamlo mkali pamoja na akina mama wenye umri wa miaka 15 hadi 49 wenye upungufu wa damu watapewa rufaa na maelezo ya mahali pa kwenda kupata huduma.

Taarifa zitakazopatikana katika utafiti huu zitaisaidia Serikali kutambua ukubwa wa tatizo la lishe duni (utapiamlo) Kitaifa na kwa kila Mkoa na hatimaye kuwezesha kupanga mipango sahihi ya kukabiliana na tatizo la lishe duni nchini. Aidha, utafiti huu utatupa mwelekeo katika utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe wa mwaka 2016/17 – 2020/21, ambao tunautekeleza kwa mwaka wa pili sasa.

Mwisho, Wizara inatoa rai kwa viongozi wote na wananchi kwa ujumla kutoa ushirikiano mzuri kwa timu za wataalam watafiti watakaopita katika kaya zenu kwa ajili ya kuendesha zoezi hili muhimu. Pia napenda kuchukua fursa hii kukanusha baadhi ya taarifa potofu au uvumi unaotolewa mitandaoni kinyume na maelezo haya ambao huenda ukatoa upotoshaji wa nia nzuri ya utafiti huu muhimu na wenye manufaa makubwa kwa taifa letu. Kwa maelezo zaidi kuhusu utafiti huu, tafadhali wasiliana na Mkurugenzi Mtendaji, Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC) inayoratibu utafiti huu: kwa Simu ya Mezani: +255 22 2118137, barua pepe: info@tfnc.go.tz au md@tfnc.go.tz na kwa Sanduku la Posta 977, Dar Es Salaam.

Imetolewa na;



Prof Muhammad Bakari Kambi

Kaimu Katibu Mkuu (Afya)

8/10/2018